# FORM FOUR CLUSTER KCSE MODEL 2

# KISWAHILI PAPER 2 ANSWER

## 1. UFAHAMU (Alama 15 )

### Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali

a) - Ana gari - Ana chumba kikubwa Ana kinasa sauti (Mziki) Ana viti vya bei ya juu (makochi)

-Ana friji

- Hupatia wageni wake vinywaji vya machungwa (Zozote 3x1 = 3mk)

b) - Ili ajue kwake na waongee zaidi kuhusu mapenzi na ndoa

- Ili waongee pasina kusumbuliwa (Yoyote lx2=2mk)

c) Alitaka kumweka tayari ili apokee habari ya mtoto aliyekuwa naye. (Alama 2)

d) Kwa sababu walikuwa wamejuana sana. (alama 2)

e) - Ni aibu kwa wazai hasa mamake.

- Alichukuliwa kama mwanaharamu. (Yoyote lx2=2mk)

f) Safari anashtuka kusikia Rehema ana mtoto ilhali yeye pia anaye na hatarajii Rehema ashtuke. (Alama 2)

g) i. Kumvisha kilemba cha ukoka= kumdanganya/kumpa sifa asizokuwa nazo. lmk.

ii. Tuliagana = Achana lmk

iii. Kwa dhati = kwa bidii/ nguvu/ kweli/ moyo mmoja. lmk

## 2. UFUPISHO (Alama 15 )

### Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali

1. Watembeao kwa miguu huhatarisha usalama kwa kuvukia kusikofaa au kutembea barabarani.
2. Wanaosukuma rukwama hukosa kufuata mkondo sahihi.
3. Waendeshaji baiskeli hukatalia barabarani licha ya kupigiwa honi.
4. Wanaoendesha pikipiki za kubeba abiria hukosa kupata mafunzo mwafaka kuhusiana na uendeshaji huo.
5. Madereva wa magari huendesha kwa kasi
6. Hupakia abiria au mizigo kupita kiasi
7. Hutumia rununu wanapoendesha au huendesha magari mabovu
8. Wanaomiliki magari ya usafiri wa umma hupuuza utunzaji wa magari hayo.
9. Huwashinikiza wahudumu kwenda kasi ili wawahi safari nyingi.

1. Ukaguzi mkamilifu ufanywe mara kwa mara.

2. Mashiriki ya bima yahimizwe kutoa vihimizo

3. Gharama za bima na za vipuli zipunguzwe.

4. Abiria wasiingie magari yaliyojaa wala kukubali kuendeshwa kwa kasi.

## 3. MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40 )

a i. Ala tuli- meno, ufizi, kaakaa gumu, kaakaa laini, koromeo

ii. Ala sogezi - Ulimi, midomo kutaja ½ mfano ½ (2x1=2)

b i. Huzuni - 1-1 alama 1

Nomino dhahania alama 1

ii. Uji - U-U alama 1 Nomino ya wingi. alama 1

c i) Kirai ni neno au fungu la maneno lisilodhihirisha maana kikamilifu.(alama 1)
ii) Wezi hao- kirai nomino Kando ya barabara - kirai kihusishi/ husishi. (2x1=2)

d Nilimwona simba mwenye watoto. (Alama 1)

e i) Mofimu ni kipashio kidogo zaidi katika lugha kilicho na maana. (Alama 1)

i) Mofimu ni kipashio kidogo zaidi katika lugha kilicho na maana. (Alama 1)

ii) Wa- li - (viambishi awali)

An - a (viambishi tamati)

f Alimjibu kuwa asingeenda ½ sokoni siku ½ hiyo ½ ila/ bali angeenda kesho ½ yake/ siku ambayo ingefuata. (alama 2)

g Mshazari hutumika:

1. Kuandika tarehe, K.m 23/3/2016

2. Kuandika visawe, K.m uki /asali

3 Kuleta dhana ya "au" mf

Nunua kondoo/ mbuzi (2x1=2)

h Kipanga ala kuku (Alama 1)

i Kinginecho kitanunuliwa. (Alama 1)

j Mgeni alipokewa na mwenyeji wake leo alfajiri. (1x2=2)

k Vitate:

sabuni - aina fulani yamchanganyiko wa madini ni mafuta ambayo hutumiwa kuogea, kusafishia au kufulia nguo.
Zabuni- i) Ni kuuza au kununua vitu kwa ushindani wa bei. (mnadani)

ii) Utaratibu wa kuuza au kununua bidhaa kwa muda maalum;tenda
* Sentensi lazima iwe moja. (1x2=2)

l Watu wachache huchukia pesa.

m

| S | | | | |
|---|---|---|---|---|
| KN | | KT | | |
| $\theta$ | I | N | S | E |
| | Nilimwona | Mamba | Niliyemwogopa sana | Majini |

n i) mhariri - shamirisho kitondo

ii) barua - shamirisho kipozi

iii) vizuri sana – chagizo

iv) kalamu ya mate- shamirisho alama (4x 12 =2).

o i) Jitu - kiambishi cha ngeli ya li-ya/ukubwa

ii) Kujilia - kirejeshi

iii) Mkimbiaji - mazoea (nomino ya mtendaji)

iv) Jino - ngeli ya LI-YA (4x½=2)

p Piga kamsa: - kupiga kelele kuonyesha hatari. (lxl =1)

q Kina: i) Silabi ya mwisho kwenye kipande cha shairi.

ii) Neno la kuelezea watu wenye uhusiano wa ukoo, jinsia na tabia mf kina mama.

iii)Urefu wa kwenda chini, K.m shimo au maji mengi. (za kwanza 2x1=2)

r vitawe : wale -

i) Kiashiria/ kionyeshi cha mbali.

ii) Kutia chakula mdomoni kiteremke hadi hadi tumboni (2x1=2)

s i) Pilipili usiyoila yakuwashiani?

ii) Mzifo u kichwani kwapa lakutokeani jasho?

iii) Mavi usiyoyala wayawingiani kuku (1x2=2)

## 4. ISIMUJAMII: (Alama 10 )

a) i)______: Ni pijini ambayo imekomaa (na kuwa lugha kamili)

ii) _______: Ni maneno/ misemo ambayo huzuka katika lugha na kutoweka baada ya muda fulani.
Au.
: Ni maneno/ misemo ambayo huzuka katika lugha na hudumu kwa muda mfupi.

iii) _____________: Ni lugha ambayo hutumiwa na watu mahsusi na katika mazingira

Fulani tu. Lugha hii huwa mwiko kwa sababu ya kuibua hisia mbaya. (3xl=alama 3)

b) ____________________

1. Lugha ya kujisifu. K.m Mimi tu ndiye mbunge tosha katika kaunti hii.

2. Sentensi huwa ndefundefu. Hasa mwanasiasa anapohutubia umati ili ajieleze zaidi.

3. Huchanganya ndimi/msimbo/ lugha mseto. K.m, Tusilete mabo ya politics katika funerals.

4. Huhamisha msimbo. K.m. I am not happy with insecurity issues in the country. Hata hivyo tukishikana mikono tutashinda tatizo hili sugu.

5. Lugha ya heshima. K.m Namkaribisha Mheshimiwa Dima atuhutubie.

6. Maswali na majibu/ huulizana na kujibizana. Mwanasiasa: Mtanipigia kura? Watu: Ndiyo.

7. Lugha ya kushawishi/ pembeleza. K.m Nipatie kura zenu na hamtajuta

. 8. Lugha ya hotuba. Wanasiasa mara nyingi huongea kwa watu njia ya hotuba.

9. Msamiati wa siasa/ teule. K.m. bunge, serikali,nk.

10. Lugha ya ahadi K.m. Mwezi ujao nitaanza kujenga barabara ya lami kutoka Sikhendu hadi Turbo.

11. Lugha ya mafumbo.k.m Mimi ni mbwa ambaye hana minofu miguuni. (Kumaanisha kuwa atakuwa mwepesi kufikia watu au ofisi zingine haraka)

12. Lugha ya kuonya/kutahadharisha K.m. Msipopiga kura vizuri mtaendelea kuumia hadi miaka mitano iishe.

13. Lugha ya vitisho K.m. Bwana Nangwe anajua matusi tu. Tutakutana kortini.

14. Lugha ya urudiaji/ uradidi/ takriri. K.m ODM chungwa! Chungwa! Chungwa!

15. Lugha ya utohozi. K.m. Spika, seneta, kaunti, nk. 16. Lugha ya ishara. K.m. Watu kuinua kidole kimoja au viwili kuashiria chama fulani.

17. Hukatizwa kauli/kalima/uneni. makofi, hoi na nderemo ya raia hukatiza hotuba ya mwanasiasa.

18. Lugha ya kejeli/ matusi/ madharau. K.m. Mkimchagua mwanafulani mashamba yenu yataenda. Yeye hupenda mashamba sana.

19. Matumizi ya vifupisho, K.m. MCA, JAP, CORD, nk

20. Lugha isiyozingatia sarufi. K.m.Mimi inakuja leo kumwelezea fainda ya ukatusi (zozote 7x1, kutaja + mfano/ maelezo = Alama 7)

- Sahihisha hoja saba za mwanzo pekee
- Mtahiniwa apewe 0 mk kwa hoja ambayo mfano wake hauafiki
- Mtahini akadirie majibu mengine